**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1017

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Mitaala na Ufundishaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-745-6

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Mitaala na Ufundishaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA MITAALA NA UFUNDISHAJI STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-745-6

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168 /+255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Mitaala na Ufundishaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

## Yaliyomo


Orodha ya Majedwali .......... iv
Vifupisho .......... v
Shukurani .......... vi
1.0 Utangulizi .......... 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania .......... 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu .......... 2
    3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu .......... 2
    3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu .......... 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu .......... 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi .......... 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 3
    6.1 Mkufunzi .......... 3
    6.2 Mwalimu Tarajali .......... 4
    6.3 Mzazi/Mlezi .......... 4
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 4
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 5
9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji .......... 5
10.0 Idadi ya Vipindi .......... 6
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji .......... 6
Bibliografia .......... 10

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3
Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu ........ 6
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Mwaka wa Kwanza ........ 7

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

## Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa somo la Mitaala na Ufundishaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za kiserikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya kusimamia kazi ya maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la maboresho ya Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Mitaala na Ufundishaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi linamwezesha mwalimu tarajali kuwa na uwezo wa kumudu mtaala wa Elimu ya Msingi, kuchambua mtaala na masuala mtambuka pamoja na kutafsiri mtaala huo katika ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, somo hili linalenga kumwezesha mwalimu tarajali kumudu maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kuwa mbunifu, mnyumbufu na mwenye uwezo wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi.

Muhtasari huu umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa Mitaala na Ufundishaji ngazi ya stashahada ya Elimu ya Msingi Tanzania Bara. Aidha, muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Muhtasari unatoa maelekezo ya kuwawezesha wakufunzi kuandaa mchakato wa ufundishaji na ujifuzaji kwa walimu tarajali kwa ufanisi. Mchakato huo wa ufundishaji na ujifuzaji unajumuisha kutumia mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji, kuandaa somo pamoja na kuandaa zana za kufundishia.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwandaa mwalimu kuwa mahiri katika:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;
(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;
(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na
(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-based action research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwalimu tarajali ni:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kutambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (instructional leadership); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-based action research*).

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa somo la Mitaala na Ufundishaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyojitokeza katika Jedwali namba 1.

**Jedwali Na. 1**:*Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu Mtaala wa Elimu ya Msingi | 1.1 Kuchambua Mtaala wa Elimu ya Msingi na vifaa vyake<br>1.2 Kuchambua masuala mtambuka katika elimu<br>1.3 Kutafsiri mtaala katika programu ya ufundishaji na ujifunzaji |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni haya yafuatayo:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;
(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na
(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

### 6.2 Mwalimu Tarajali

Mwalimu tarajali anatarajiwa

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za kufundishia na kujifunzia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini mwanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

### 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi /mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi umejikita katika maarifa, stadi na mwelekeo. Mwalimu tarajali anatarajiwa kupata maarifa kuhusu Elimu ya Msingi na kutumia muda mwingi kufanya mazoezi kwa vitendo kutokana na maarifa aliyoyapata. Mkufunzi anapaswa kutumia mbinu shirikishi zitakazomwezesha mwalimu tarajali kujenga umahiri uliokusudiwa. Mbinu zinazopendekezwa kutumika katika muhtasari ni zile zinazomshirikisha mwalimu tarajali katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji anuai na uwezo wake. Mbinu hizo ni kama vile nyimbo, hadithi, michezo, onesho mbinu, matembezi ya galari, igizodhima, ziara ya mafunzo na majadiliano katika vikundi. Vilevile, mbinu hizi

zitamwezesha mwalimu tarajali kuwa mbunifu, kufikiri kiyakinifu, kuwasiliana, kushirikiana, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kutatua changamoto mbalimbali katika maisha yake ya kila siku. Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na kufaragua zana za ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia mazingira halisi ya mwanafunzi.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji na uwezo wa mwalimu tarajali. Aidha, zana za ujifunzaji na ufundishaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kumudu kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka. Zana za ujifunzaji na ufundishaji zinazopendekezwa ni pamoja na kompyuta, printa, tableti zenye somo husika, diski, matini zenye vifungu vya habari vinavyohusiana na umahiri unaohusika, matini za kibunifu na zisizo za kibunifu, michoro, picha, kinasasauti, televisheni, filamu, redio, vitu halisi, na kamusi.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Upimaji wa somo la Mitaala na Ufundishaji utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya Elimu ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi. Upimaji huu utamwezesha mkufunzi kupima umahiri wa mwalimu tarajali wa kuchambua Mtaala wa Elimu ya Msingi. Aidha, utamwezesha mkufunzi kubaini uwezo wa mwalimu tarajali wa kuchambua vifaa vya mtaala katika kuandaa programu ya ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa maendeleo utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwa hiyo, zana zinazotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, majaribio, majaribio kwa vitendo, hojaji, uwasilishaji, mkoba wa kazi, kazimradi, mitihani ya muhula, na mtihani wa mwisho.

Katika kuamua kiwango cha ufaulu wa mwalimu tarajali upimaji wa mwisho (tamati) utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini (50%) na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha asili mia hamsini (50%), mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli za upimaji | Mgawanyo (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Muhula wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi Mradi | 7.0 |
| **5** | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa somo la Mitaala na Ufundishaji Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi viwili (2) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya muhtasari huu yamegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo ni: Umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana na idadi ya vipindi kama Jedwali namba 3 linavyoonesha.

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahsusi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu Mtaala wa Elimu ya Msingi | 1.1 Kuchambua mtaala wa Elimu ya Msingi na vifaa vyake | Kuchambua mtaala wa Elimu ya Msingi na vifaa vyake (maana, aina za mtaala, umuhimu na vipengele vya mtaala), (muhtasari, kitabu cha kiada, kiongozi cha mwalimu, vitabu vya ziada) | Mtaala wa Elimu ya Msingi na vifaa vyake umechambuliwa | Mtaala wa Elimu ya Msingi, mihstasari ya masomo yanayohusika, kitabu cha kiada, kiongozi cha mwalimu, vitabu vya ziada, projekta na kompyuta | 22 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahsusi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kuchambua masuala mtambuka katika Mtaala wa Elimu ya Msingi | Kubainisha masuala mtambuka katika Mtaala wa Elimu ya Msingi na kuhusianisha na masomo bebezi | Masuala mtambuka katika Mtaala wa Elimu ya Msingi yamebainishwa | Mtaala wa Elimu ya Msingi, kitabu cha kiada, vitabu vya ziada, video zenye masuala mtambuka, projekta, filamu zenye masuala mtambuka, makala na matini zenye masuala mtambuka, sidii zenye masuala mtambuka, tableti zenye masuala mtambuka na simujanja zenye masuala mtambuka | 19 |
| | 1.3 Kutafsiri mtaala katika programu ya ufundishaji na ujifunzaji | Kumudu stadi za kuandaa mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji na katika Elimu ya Msingi unaozingatia | Stadi za kuandaa mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa umahiri zimebainishwa | Muhtasari wa somo linalohusika, kitabu cha kiada, vitabu vya ziada, ratiba ya mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, kalenda ya mwaka na ya shule yenye mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji na | 29 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahsusi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ujenzi wa umahiri (azimio la kazi, andalio la somo, nukuu za somo na shajara ya somo) | | ujifunzaji, miongozo mbalimbali yenye mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, moduli za mwalimu tarajali, kompyuta, tableti zenye mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji, simujanja zenye mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji na sidii zenye mpango wa kutayarisha vifaa vya ufundishaji | |

## Bibliografia


David, N., & Robert, C. (1995). *A handbook for teachers in the university and college: A guide to improving teaching methods*. Kogan Page.

Erickson, H.L (2007). *Concept based curriculum and instruction: Teaching beyond facts.* Corwin Press. INC.

Kitta, S., & Tilya, F. N. (2010). The Status of Learner-Centred Learning and Assessment in Tanzania in the Context of the Competence-Based Curriculum. *Papers in Education and Development,* 29, 77-91.

Makulel, J. C. (1998). *Creative approaches to classroom teaching*. Discovery Publishing.

Marsh, C. J. (1997). *Perspectives: Key concepts for understanding curriculum*. Falmer.

Ministry of Education and Culture. (1995). *Education and training policy*. Ministry of Education and Culture.

Ministry of Education and Culture. (2009). *Curriculum and teaching syllabus for diploma in education*. Tanzania Institute of Education.

Ministry of Education and Vocational Training. (2007). *Foundations of education syllabus for diploma in secondary education*. Ministry of Education and Vocational Training.

Ministry of Education Vocational and Training. (2014). *Education and training policy*. Ministry of Education Vocational and Training.

Neary, M. (2002). *Curriculum studies in post-compulsory and adult education: A teacher's and student teacher's study guide*. Nelson Thornes Ltd.

Posner, G. J. (1995). *Theoretical perspectives on curriculum.* MA: Pearson Custom Publishing.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2003). *Moduli ya somo la misingi ya elimu: Mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Tanzania Institute of Education. (2013). *Module of curriculum and teaching diploma in secondary education curriculum.* Tanzania Institute of Education.

Tanzania Institute of Education. (2015). *Guideline for evaluation of books*. Tanzania Institute of Education.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2014). *Sera ya elimu na mafunzo.* Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Mtaala wa mafunzo ya stashahada ya ualimu elimu ya awali.* Taasisi ya Elimu Tanzania.